

ksh. 3,000

TAHARUKI NA SADFA KATIKA UJENZI WA MAUDHUI KATIKA
RIWAYA ZA MWANA WA YUNGI HULEWA NA TUTARUDI NA ROHO
ZETU

NA

CHRISTOPHER ORINA/MAROKO

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA
LUGHA ZA KIAFRIKA KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA
KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA

SHAHADA YA UZAMILI

Maroko, Christopher Orina
*Taharuki na sadfa katika
ujenzi wa maudhui katika*




JUNI, 2022

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Ungano

Tasniifu hii ni kazi yangu asili wala haijupata kowasilishwa katika chuo kikuu
chochote kwa minajili ya shahada yoyote.

Sahihii 


Tarehe 21.06.2022

CHRISTOPHER ORINA MAROKO

C50/CE/22441/2011

Idhini

Tasniifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo
kikuu.


Sahihii 

Tarehe 21/06/2022

DKT. MIRIAM KENYANI OSORE

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Sahihii 

Tarehe 21/06/2022

DKT. DAVID KIHARA

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Shukrani

Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, hekima na maarifa katika safari hii ya uandishi wa tasnifu hii ya uzamili.

Vile vile ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt. Miriam Kenyani Osore na Dkt. David Kihara kwa kuniongoza na kunielekeza bila kuchoka. Maelekezi yenu yalinifaa sana.

Namshukuru babangu mzazi, Maroko Obare kwa kunipa motisha ya kuanza, kuendelea na kumaliza masomo yangu kufikia kiwango hiki.

Ningependa pia kumshukuru mke wangu, Mercy Musa kwa kunipa hima na motisha ya kumaliza tasnifu hii. Maombi yako yalinifaa sana katika safari hii. Mwisho, namshukuru Meshack Munyao kwa kunifaa katika uandishi wa tasnifu yangu. Mungu akubariki.

Ikisiri

Utafiti huu ulishughulikia matumizi ya taharuki na sadfa katika ujenzi wa maudhui katika riwaya za *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) na *Tutarudi na Roho Zetu* (1987) zilizoandikwa na Muhammed Said Abdulla na Ben Mtobwa mtawalia. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza namna taharuki na sadfa zimetumika kujenga maudhui ya riwaya teule. Malengo ya utafiti yalikuwa kubainisha aina za taharuki zilizotumika katika riwaya teule, kuchanganua aina za sadfa zilizotumika katika riwaya teule na maudhui yaliyojengwa katika riwaya za *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) na *Tutarudi na Roho Zetu* (1987). Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki wa kimtindo kwa mujibu wa Leech (1969). Nadharia ya uhakiki wa kimtindo huchunguza namna mtindo hutumiwa na mtunzi katika kujenga maudhui. Katika utafiti huu, mbinu kusudio ilitumika kuteua aina za taharuki na aina za sadfa zilizotumiwa katika riwaya teule. Aidha, maudhui yaliyojengwa katika riwaya teule yaliangaziwa. Data iliyochanganuliwa ilipatikana kwa kusoma riwaya teule. Data hii ilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya uhakiki wa kimtindo kwa kuainisha na kuchanganua aina za taharuki na aina za sadfa zilizotumika na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Uchunguzi huu ulibainisha kuwa: taharuki na sadfa ni muhimu katika kujenga maudhui ya riwaya za kipelelezi, taharuki hutanguliza maudhui yanayoandikiwa na huibua masuala halisi katika jamiina sadfa hupelekea riwaya za kipelelezi kiafikia kilele chake. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa utasaidia wanaosoma kuelewa kuwa taharuki na sadfa huweza kuainishwa kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Aidha uchunguzi huu utasaidia kufahamu namna taharuki na sadfa zimetumika kujenga maudhui katika riwaya za kipelelezi.

Abstract

This study aims at analyzing the utilization of suspense and coincidence in bringing out themes in *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) and *Tutarudi na Roho Zetu* (1987) by Muhammed Said Abdulla and Ben Mtobwa respectively. This study aimed at analyzing how types of suspense and types of coincidence brings out themes in the selected novels. The objectives of the research are to analyze the types of suspense and types of coincidence and show how they are utilized in the selected novels and to examine themes in the selected texts. This study was guided by the theory of stylistics as elaborated by Leech (1969). Stylistics investigates how features of style are utilized in bringing out themes by the writer. In this study, purposive sampling was used in identifying instances in which the reader is left in mental uncertainty and anxiety awaiting an outcome of an occurrence. Besides, the instances that lead to the unfolding of events that act as pointers of evidence of what is under investigation was analyzed. The data that was analyzed was obtained from reading the selected novels. The data was analyzed in line with the tenets of theory of stylistics by categorizing types of suspense and coincidences, analyzing and evaluating their significance and the findings was presented in form of discussion. The study found out that: Suspense and coincidence are important in bringing out themes in the selected novels, suspense introduces the themes in question, suspense brings out themes concerning real issues in society, there is a relationship between suspense and coincidence and coincidence leads to the climax of the novel. The study is important for it will help readers to understand that suspense and coincidence can be categorized according to different writers. Besides, this study will help in understanding suspense and coincidences and how they bring out themes in investigative novels.

Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu

Taharuki - Hali ya matarajio ambapo msomaji au mtazamaji wa kazi ya fasihi huwa na hamu ya kutaka kujua kitakachotokea baada ya matukio fulani. Huenda matokeo hayo yametarajiwa kutokea kwa namna fulani lakini yakatokea kinyume na matarajio hayo au hayakutarajiwa kutokea lakini yakatokea.

Sadfa- Ni utokeaji wa matukio mawili au zaidi yaliyo na uhusiano fulani kwa wakati mmoja na aghalabu bila kupangwa au kutarajiwa kutokea. Matukio haya aghalabu hupangwa na mwandishi wa kazi ya fasihi.

Bunilizi- Aina ya fasihi andishi inayojengeka kwa masimulizi.

Riwaya za kipelelezi- Aina za riwaya zinazoshughulikia uovu au uhalifu, mapenzi, jinai na dhuluma, na mhusika mkuu hupeleleza maovu yanayoendelezwa riwayani kwa kuunga vielekezi vinavyopelekea ugunduzi wa aliyesababisha maovu hayo.

Mtindo- Ni namna mwandishi hutumia lugha kupitisha ujumbe katika kazi ya fasihi. Husaidia kueleza wazo na dhamira ya mwandishi na kusarifu kazi nzima ya fasihi ili kufanikisha ufasaha wa kazi ya fasihi. Mtindo huhusisha taharuki, sadfa, taswira, tasfida, jazanda, viangaza mbele, tashtiti na takriri.

Aporia- Suala ambalo haliwezi kuamuliwa kimantiki katika kazi ya fasihi au analokabiliana nalo msomaji. Mgogoro usiosuluhika unaomweka msomaji wa kazi ya fasihi katika hali ya kutoweza kufanya uamuzi wowote.

Mshtukizo- Ni hali ambapo si rahisi kutabiri matukio fulani au utokeaji wake.

Yaliyomo

Ungamo.....	iii
Shukrani	iii
Ikisiri.....	iv
Abstract.....	v
Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu.....	vi
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 Usuli wa Utafiti.....	1
1.1 Suala la Utafiti.....	8
1.2 Malengo ya Utafiti	10
1.3 Maswali ya Utafiti	10
1.4 Sababu za Kuchagua Mada	10
1.5 Upeo na Mipaka.....	14
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	15
1.7 Misingi ya Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo.....	22
1.8 Mbinu za Utafiti	24
1.8.1 Muundo wa Utafiti.....	25
1.8.2 Mahali pa Utafiti	25
1.8.3 Uteuzi wa Sampull	26
1.8.4 Ukusanyaji wa Data.....	26
1.8.5 Uchanganuzi wa Data	27
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo	28
SURA YA PILI.....	29
AINA ZA TAHARUKI ZILIZOTUMIKA KATIKA RIWAYA ZA MWANA WA YUNGI HULEWA NA TUTARUDI NA ROHO ZETU.....	29

2.0 Utangulizi	29
2.1 Taharuki katika Riwaya Teule	30
2.2 Taharuki za Ulimbende katika Riwaya Teule.....	34
2.3 Taharuki za Mwigo Zilivyotumika Katika Riwaya Teule	47
2.4 Taharuki za Kutisha katika Riwaya Teule	55
2.5 Hitimisho	65
SURA YA TATU.....	67
<i>AINA ZA SADFA KATIKA RIWAYA ZA MWANA WA YUNGI HULEWA (1976) NA TUTARUDI NA ROHO ZETU (1984)</i>	67
3.0 Utangulizi	67
3.1 Nafasi ya Sadfa katika Riwaya Teule.....	70
3.1.1 Sadfa Zinazotokea Mfululizo Katika Riwaya Teule.....	72
3.1.2 Sadfa ya Kushtuza Inayoḡrudia Katika Riwaya Teule.....	78
3.1.3 Sadfa ya Usambamba wa Maisha Katika Riwaya Teule	80
3.1.4 Sadfa ya Kutatanisha Isiyoeleweka Katika Riwaya Teule.....	83
3.1.4.1 Sadfa ya Kutatanisha Kijiografia.....	83
3.1.4.2 Sadfa ya Kutatanisha Kiteknolojia.....	89
3.1.5 Sadfa ya Mfululizo wa Matukio Yasiyotarajiwa Katika Riwaya Teule	93
3.2 Hitimisho	97
SURA YA NNE	100
<i>MAUDHUI YALIYOJENGWA NA TAHARUKI NA SADFA KATIKA RIWAYA ZA MWANA WA YUNGI HULEWA (1976) NA TUTARUDI NA ROHO ZETU (1984)</i>	100
4.0 Utangulizi	100
4.1 Maudhui ya Mauaji	101
4.2 Maudhui ya Uongo.....	104

4.3 Maudhui ya Nafasi ya Mwanamke Katika Jamil.....	106
4.4 Maudhui ya Ubadhirifu	108
4.5 Hitimisho.....	109
SURA YA TANO.....	111
MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA MCHANGO WA UTAFITI	111
5.0 Utangulizi	111
5.1 Matokeo ya Utafiti	113
5. 2 Mchango wa Utafiti.....	115
5.3 Mapendekezo ya Utafiti.....	116
MAREJELEO	118